**HOTUBA YA WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI,
MHE. MUSTAFA HAIDI MKULO (MB), WAKATI AKIFUNGUA
MKUTANO WA BARAZA LA WAFANYAKAZI WA WIZARA YA FEDHA
NA UCHUMI TAREHE 16 – 17 DESEMBA, 2009 – MBEYA**

Bw. Ramadhani Khijjah, *Katibu Mkuu na Mwenyekiti wa Baraza la Wafanyakazi wa Wizara ya Fedha na Uchumi;*

Bw. John M. Haule, *Naibu Katibu Mkuu, Wizara ya Fedha na Uchumi;*

Dr. Phillip Mpango, *Naibu Katibu Mkuu, Wizara ya Fedha na Uchumi;*

Bw. Cyprian Kuyava,
Katibu wa Baraza la Wafanyakazi Wizara ya Fedha na Uchumi;

Wajumbe wa Baraza la Wafanyakazi;

Mabibi na Mabwana;

Asalaam Aleykum!

1. ***Ndugu Mwenyekiti,*** awali ya yote naomba nianze kwa kumshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kusafiri salama, kutujalia afya njema na kutuwezesha kukutana leo katika Kikao cha Baraza la Wafanyakazi ambacho kwa mara ya kwanza kinafanyika hapa mkoani Mbeya.

2. Pili, napenda nikushukuru wewe Ndugu Mwenyekiti na Kamati yako kwa kunialika kuwa Mgeni rasmi katika kikao hiki na pia kwa kufanikisha

maandalizi ya Kikao hiki muhimu kwa watumishi wa Wizara ya Fedha na Uchumi. Kama mnavyofahamu kuwa lengo kuu la Mabaraza ya Wafanyakazi sehemu za kazi ni kuongeza tija na kuleta ufanisi katika taasisi kwa kuwashirikisha wafanyakazi katika uongozi wa pamoja mahali pa kazi kama linavyoagiza agizo la Rais *Na. 1 la mwaka 1970,* likisomwa pamoja na miongozo mingine inayotekeleza agizo hilo.

3. ***Ndugu Mwenyekiti,*** nimejulishwa kuwa katika mkutano huu pamoja na mada mbalimbali zitakazowakilishwa zipo mada ambazo zitaelezea majukumu ya Idara zilizo chini ya Wizara ya Fedha na Uchumi. Mada hizi zilipendekezwa kutokana na umuhimu wake ili kuwawezesha Wajumbe kufahamu majukumu yanayofanywa na idara zetu. Mada ambazo nimefahamishwa kuwa zitawasilishwa na kujadiliwa ni pamoja na:-

- *Usalama wa Serikali pamoja na upekuzi.*
- *Rushwa, Uwazi na Uwajibikaji*.
- *Mikakati ya ukusanyaji wa mapato ya ndani ili kuendeleza Uchumi.*
- *Dhima ya Menejimenti ya Maafa.*
- *Matumizi bora na salama ya vifaa na mifumo ya kompyuta.*
- *Majukumu na Changamoto ya Sera ya Ununuzi wa Umma.*

- *Maendeleo ya Utumishi na Mafunzo.*
- *Muundo wa Wizara na changamoto.*
- *Ajali, fidia na changamoto zake.*

4. **Ndugu Mwenyekiti,** Mkutano wetu wa Baraza la Wafanyakazi unafanyika katika kipindi ambacho Serikali iko katika Mkakati wa utekelezaji wa Kauli Mbiu ya "***Kilimo Kwanza",*** ambayo imeainishwa kwenye Bajeti ya serekali ya mwaka 2009/10. Katika kutekeleza kauli mbiu hii, Wizara ya Fedha na Uchumi inalojukumu la kutekeleza nguzo ya pili ya "Kilimo kwanza" ambayo inahusu ugharamiaji wake. Kwa kutekeleza jukumu hilo, kwa mwaka 2009/10, tayari mfuko wa maendeleo ya Kilimo ya Kimataifa (**IFAD**) na Benki ya Maendeleo ya Afrika (**ADB**) wameisaidia Tanzania kwa kutoa Dola za Kimarekani 24 millioni katika mradi wa ASDP. Kadhalika Benki ya Dunia wanasaidia mradi huu ili kuhakikisha upatikanaji wa chakula (Accelerated Food Security) kwa kiasi cha Dola za Kimarekani 160 millioni.

5. Katika Bajeti ya Serikali ya mwaka 2010/11, Wizara imehakikisha kuwa sekta ya kilimo itatengewa asilimia 10% ya Bajeti ya Serikali. Aidha, Kamati ya Mwongozo wa Mpango wa Bajeti ya mwaka 2010/11 – 2012/13 itakuwa na mwakilishi kutoka Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika.

6. ***Ndugu Mwenyekiti,*** kama mnavyofahamu Serikali imechukuwa hatua mbalimbali katika kukabiliana na athari za kuporomoka kwa uchumi duniani. Hatua hizo ni pamoja na kutenga kiasi cha shilingi 1.7 trilioni katika bajeti ya Serikali ya mwaka 2009/10 kwa ajili ya kunusuru uchumi wa Tanzania.

7. Kadhalika, Serikali imetoa shilingi 20 bilioni kwa Bodi ya Pamba ili kufidia upungufu wa bei katika msimu huu. Aidha, kiasi cha shilingi 20 bilioni nyingine zimetengwa kwa ajili ya kuboresha na kupanua mifuko ya kudhamini mikopo ikijumuisha Export Credit Guarantee Scheme (ECGS) na Small and Medium Enterprises Schemes (SMES).

8. Pamoja na hayo, kiasi cha shilingi 141 bilioni kimetengwa kwa ajili ya kuboresha na kuongeza uzalishaji wa chakula wa Ghala la Taifa la Chakula na kuhakikisha upatikanaji wa zana za kilimo. Katika kiasi hicho, shilingi 20 bilioni zimetumika kwa ajili ya uzalishaji wa chakula, shilingi 20 bilioni zimetumika kwa ajili ya Ghala la Taifa la Chakula, na shilingi 20 bilioni kwa ajili ya "lease financing" kupitia benki, kwa ajili ya kununulia zana za kilimo.

9. ***Ndugu Mwenyekiti,*** Nimefahamishwa kuwa kauli mbiu ya mkutano huu ni ***TUIMARISHE MIKAKATI YA UKUSANYAJI WA MAPATO YA NDANI KUENDELEZA UCHUMI.*** Wizara ya Fedha na Uchumi imepewa

jukumu la kukusanya mapato na kusimamia matumizi ya Serikali pamoja na kuimarisha uchumi tulivu. Kwa msingi huo Wizara inalo jukumu la kuandaa Sera za mapato zenye kupanua wigo na pia kukuza uchumi kwa njia ya kuongeza pato la Taifa kwa ujumla. Aidha, Wizara imeendelea kutimiza majukumu haya kwa kuimarisha ukusanyaji wa mapato, kusimamia matumizi ya fedha za umma na uwajibikaji .

10. Katika mwaka 2009/10, Serikali imeweka lengo la kukusanya mapato ya ndani yanayokadiriwa kuwa Tsh. 5,096,935 milioni. Ili kufikia lengo hilo ni wajibu wa Wizara ya Fedha na Uchumi kuongeza juhudi na kuimarisha ukusanyaji wa mapato kutoka kwenye vyanzo mbalimbali. Hatua ambazo zimechukuliwa na Serikali katika bajeti ya mwaka 2009/2010 ili kuongeza mapato haya ni pamoja na:-

- Kupanua wigo wa kodi,
- Kufanya marekebisho katika baadhi ya kodi zinazotozwa kwenye sekta ya madini,
- Kupunguza misamaha ya kodi, na
- kuendelea kusimamia ukusanyaji wa mapato yasiyo ya kodi.

11. Tayari tathimini ya utaratibu na utambuzi wa vyanzo vya mapato yasiyo ya kodi yanayokusanywa na Wizara, Mikoa na Idara zinazojitegemea imekamilika. Ripoti imewasilishwa Wizara ya Fedha na Uchumi kwa ajili ya hatua za Kisera.

12. ***Ndugu Mwenyekiti,*** hizo ni baadhi tu ya hatua ambayo Wizara imechukua ili kuongeza juhudi na kuimarisha ukusanyaji wa mapato kutoka kwenye vyanzo mbalimbali. Naomba ieleweke kwamba ni jukumu letu sote kuongeza juhudi katika ukusanyaji mapato, ili kuweza kufikia malengo tuliyojipangia na pia ni wajibu wa watendaji katika ngazi zote za Wizara na Taasisi za Serikali kubuni mikakati ya ukusanyaji wa mapato ya ndani ili tuweze kugharamia sehemu kubwa ya matumizi yetu na kupunguza utegemezi.

13. ***Ndugu Mwenyekiti,*** Wakati tulipofanya mkutano wa Baraza la Wafanyakazi mwaka huu huko Mkoani Morogoro nilizungumzia suala la uvujaji wa siri za Serikali na utendaji kazi usiokidhi viwango. Ningependa kuwakumbusha tena na ningependa tuendelee kukumbushana katika vikao vyetu vya Baraza la wafanyakazi mambo yafuatayo:-

(i) Ili Wizara iweze kutekeleza malengo iliyojiwekea, hatuna budi kila Mtumishi adhamirie kufikia kiwango cha juu cha uadilifu na uwajibikaji. Hii itatuwezesha kujenga imani kwa wadau na wananchi tunaowahudumia.

(ii) Tunahitaji kutekeleza majukumu yetu kwa kuzingatia Sheria, Kanuni na taratibu za Utumishi wa umma, kutumia utaalamu wetu kwa uaminifu, kutoa huduma bora na kutokuwa na upendeleo wakati wa kuhudumia wananchi.

(iii) Kutumia ipasavyo na kwa uangalifu taarifa tuzipatazo kutokana na majukumu tuliyonayo, kutoziacha ovyo hatimaye kuwafikia watu wasiohusika.

14. ***Ndugu Mwenyekiti,*** mwakani tunaelekea katika kipindi cha uchaguzi wa Rais na Wabunge na ni vema tukakumbushana masuala yanayotuhusu kama watumishi wa umma. Ndugu Wajumbe, Kanuni za utumishi wa umma zinaheshimu haki na uhuru wa Mtumishi wa Umma kuwa mwanachama na kukipigia kura chama chochote akipendacho. Pia Mtumishi wa Umma anaruhusiwa kushiriki katika shughuli za kisiasa ili mradi kusiwepo upendeleo kwa upande wowote katika kutekeleza majukumu kama Mtumishi wa Umma. Aidha, napenda kuwakumbusha kutotumia nyaraka au taarifa za ofisi ya

Umma kwa masuala ya kisiasa, kwani hii ni uvunjaji wa Taratibu za Utumishi wa Umma.

HITIMISHO

15. ***Ndugu Mwenyekiti na Wajumbe,*** napenda nikumbushe tena kuwa Wizara yetu inabeba majukumu makubwa sana ya kuhakikisha tunatimiza malengo ya ukusanyaji wa mapato ya ndani ili kuendeleza uchumi wetu. Hii ina maana tunao wajibu wa kuongeza tija na ufanisi katika kutekeleza jukumu hili. Napenda kuwashukuru wafanyakazi wote wa Wizara ya Fedha na Uchumi kwa jitihada zenu katika kutimiza wajibu wenu na kuhakikisha Wizara inafikia malengo tuliyojiwekea. Naamini kuwa mtatumia Mkutano huu kutathmini utendaji kazi wa Wizara, na mchango wetu katika kufikia malengo tuliyojiwekea. Ninawatakieni Mkutano wenye mafanikio makubwa.

16. ***Ndugu Mwenyekiti na Wajumbe,*** *baada ya kusema hayo, napenda kutamka sasa kuwa Mkutano huu wa Baraza la Wafanyakazi la Wizara ya Fedha na Uchumi umefunguliwa rasmi.*

Nawatakieni Krismas njema na heri ya Mwaka Mpya 2010

AHSANTENI SANA KWA KUNISIKILIZA.